**East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature**
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-7 | Issue-12 | Dec- 2024 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2024.v07i12.006

OPEN ACCESS

**Original Research Article**

# Mazingira ya Ujitokezaji wa Matendo uneni katika Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*

Edson Limbuko Andrea[1*], Dkt Neema George Mturo[2]
[1]Mwanafunzi Wa Shahada Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Tumini Makumira, Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii, Tanzania
[2]Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii, Tanzania

**Article History**
**Received:** 07.08.2024
**Accepted:** 25.11.2024
**Published**: 30.12.2024

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala haya yanahusu ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*. Lengo la Makala haya, ni kuchunguza mazingira yanayoukilia utokeaji wa matendo uneni katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*. Data za zilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi matini na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Sampuli ya utafiti ilikuwa ni tamthiliya mbili ambazo ni *Nguzo Mama* na *Kivuli Kinaishi*, sampuli hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu ya kutabakisha na mbinu ya usampulishaji vigezo. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Kitendo uneni kama ilivyoasisiwa (1962) na Austin kuendelezwa na Searle (1975). Matokeo yanaonesha kuwa, kuna mazingira maalumu yanayoukilia utokeaji na utendekaji wa matendo uneni. Mazingira hayo ni: wakati muafaka, lengo la tukio, hadhi na mamlaka ya mtoa usemi. Kadhalika, vifaa maalumu vya kufanikisha tendo uneni husika na hadhira inayoathirika na tendo uneni hilo. Kwahiyo, watafiti na wataalamu wa fasihi wanapaswa kujikita katika tanzu zote za fasihi andishi hasa kwenye tamthiliya ili kuchunguza matendo uneni na mazingira ambayo hupelekea kutokea kwa matendo uneni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba matendo uneni ni mbinu mojawapo ambayo waandishi huitumia kama ubunifu wenye kuleta tija katika tanzu za fasihi andishi.

**Keywords:** Tendo uneni, Mazingira.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Waandishi wengi wa kazi za kifasihi huibuka na njia mbalimbali za kuendeleza kazi zao, miongoni mwa njia hizo ni matumizi ya matendo uneni. Wataalamu mbalimbali akiwemo Matinde, (2012) amefafanua matendo uneni kuwa ni dhana inayoelezea jinsi mtu anavyotoa usemi au tamko fulani ambalo hupelekea kutendeka kwa jambo fulani kulinga na usemi/tamko husika. Waandishi wa kazi za kifahisi wamekuwa wakitunga na kuandika kazi zao za kifasihi kwa kuhusisha mazingira mbalimbali yanayoibua matendo uneni kama njia moja wapo ya kuzipamba kazi hizo. Matumizi ya matendo uneni kwa waandishi yanajitokeza kwa namna ambayo yanaibuka katika mazingira mbalimbali ya ujitokezaji kwa msukumo wa vitendo au usemi katika kazi za kifasihi (Resani, 2014). Matumizi ya matendo uneni na mazingira yake ya ujitokezaji yameweza kubainika zaidi kutumiwa na waandishi wa tamthiliya mbalimbali.

Kwani, tamthiliya ni mojawapo ya tanzu muhimu sana katika fasihi andishi zikiwemo tanzu nyingine kama riwaya na ushairi. Watunzi wengi wa kazi za tamthiliya hutunga kazi zao kulingana na maudhui au matukio yanayoelekeana na jamii. Aidha, hutumia njia mbalimbali za kisanii ili kufikisha ujumbe wa kile mwandishi anacho lenga kwa wanajamii. Baadhi ya waandishi hutunga tamthiliya moja kwa moja kutoka katika lugha lengwa na kazi nyingine zikiwa zimetafsiriwa kutoka katika lugha za kigeni kama: Kiingereza–Kiswahili, Kibantu-Kiswahili (Wafula, 1999). Ingawa makala haya yamejikita katika tamthiliya za waandishi wa Kiswahili ambazo hazikutafsiriwa ili kubaini ujitokezaji wa matendo uneni katika kazi hizo teule.

Hivyo, Tamthiliya huwasilishwa kwa mazungumzo ya majibizano na matendo kwa pamoja. Matendo na mazungumzo hayo hudhihirika kama matendo uneni ambayo hutokana na mazingira mbalimbali. Mfano wa mazingira hayo ni: lengo la mtoaji usemi na hadhi na mamlaka ya mtoa usemi (Raseni, 2014). Hoja hii imeweza kushabiana na utafiti wa Walya (1995) alipochunguza usemi utumikao benki na watumishi wa benki wanapowasiliana na wateja wao. Katika uchanganuzi wake alibaini kuwa kuna athari

***Corresponding Author:** Edson Limbuko Andrea
Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Tumini Makumira, Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii, Tanzania

chanya katika semi zituwiwazo na wafanyakazi wa benki kwa wateja wao. Pia, alionesha kuwa wafanyakazi wa benki hutumia lugha kwa kutamka jambo na kutenda kwa kutumia lugha ya ishara kwa nia ya kupata wateja na kuwashawishi waweze kufurahia huduma zao. Utafiti huu umejikita katika muktadha wa kibenki, hivyo utafiti wa sasa unatalii katika matini andishi.

Matasi (2014) alichunguza vitendo uneni katika khutuba za ijumaa na athari zake kwa waumini wa bugisi, Mashariki mwa Uganda. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa khutuba za ijumaa zina matendo uneni maalum ambayo yanaathari hasi kwa waumini wanaosikiliza khutuba. Utafiti wa Matasi (kshtj) ulijikita katika kuchunguza matendo uneni katika khutuba za ijumaa, lakini utafiti huu umechunguza matendo uneni katika utanzu wa tamthiliya.

Vilevile Ogolla, (2007) alichunguza namna lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao, lengo lilikuwa ni kubainisha vitendo neni vinavyojitokeza katika matamko ya kuwahamasisha wanawake na jinsi wanavyoweza kuathirika nayo. Utafiti wake ulionyesha kwamba lugha inayotumika wakati wa uhamasishaji wa wanawake ina vitendo uneni na athari chanya kwa wasikilizaji. Hata hivyo, utafiti wa Ogolla (Kshtj) ulijikita katika kuchunguza vitendo uneni katika matamko ya kuwahamasisha wanawake ilhali utafiti wa sasa ulichunguza matendo uneni katika tamthiliya.

Aidha, pamoja na kwamba tafiti tangulizi zimehusisha dhana ya matendo uneni katika muktadha halisi kama vile katika khotuba na miktadha ya Benki. Swali la kujiuliza ni kwamba matendo uneni hudhihirika katika muktadha halisi tu au hata katika muktadha ambao si halisi? Pia, kama yapo ni mazingira gani ambayo hupelekea matendo uneni hayo kuwepo? Hivyo basi, imeonekana kuna haja ya kuchunguza mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika muktadha ambao si halisi. Kwa mfano; utanzu wa tamthiliya hutumia muktadha ambao si halisi ambao hujikita katika lugha ya mazungumzo yenye kuambatana na matendo mbalimbali. Hii ni sifa anuai ya utanzi wa tamthiliya ambayo hutumia wahusika katika kunena na kutenda hali ambayo huweza kuibua matendo uneni mbalimbali.

Hivyo basi, kwa kutumia nadharia ya kiteno uneni iliyoasisiwa mwaka wa 1962 na Austin. Makala haya yamekusudia kuchanganua mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*, kwa lengo la kuonesha kwamba sio tu katika mikutadha halisi ndipo matendo uneni hudhihirika bali pia hata katika muktadha ambao sio halisi kuna mazingira ambayo huweza kupelekea matendo uneni kujitokeza.

## 2.0 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mbinu mbalimbali zilizotumika kufanikisha kazi hii. Ambazo ni pamoja na mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango, usampulishaji, sampuli, mbinu za ukusanyaji data na uchanganuzi wa data.

### 2.1 Mkabala, Usanifu, Eneo, Wango, Usampulishaji, Sampuli

Makala hii imetumia mkabala wa kimaelezo kwani ni mkabala unaojikita katika maoni ya watoa taarifa. Mkabala huu umemuwezesha mtafiti kupata ufafanuzi na maelezo ya kina kuhusu mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni. Kadhalika, mkabala huu umemuwezesha mtafiti kuchanganua data na kuandika malaka inayofafanua vyema mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya teule.

Aidha, makala hii imeongozwa na usanifu wa kifani kwa lengo la kuchanganua mazingira yaliyopelekea kujitokeza kwa matendo uneni katika tamthiliya teule. Pia, makala hii imehusisha sampuli mbili: tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*, ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya kutabakisha na mbinu ya usampulishaji vigezo. Aidha, katika mbinu hii mtafiti alijiundia kanuni ya kufanya utafiti wa awali kwa kusoma tamthiliya zote za mwandishi Mohamed na Penina, kwa kujiwekea vigezo ambavyo vimezingatiwa kwanza, matini andishi yenye lugha ya mazungumzo, pili, matini rasmi na tatu tamthiliya ambayo ilidhihirisha kuwepo kwa matendo uneni mengi kuliko nyingine ndo iliteuliwa kuwa sampuli ya utafiti huu.

### 2.2 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data na Uchambuzi wa Data

Data za makala haya zilikusanywa kutoka maktabani. Aidha, mbinu ya uchanganuzi matini imetumika kwa kusoma tamthiliya teule. Pia, data zimechanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kusimbisha maudhui. Katika makala haya mtafiti amezingatia hatua za uchanganuzi wa data. Kwanza, kuzizoea data kwa kuzisoma data ambazo zimekusanywa kutoka katika tamthiliya teule. Pili, mtafiti alitengeneza misimbo mbalimbali kwa kuzingatia malengo mahususi, matukio, mipango, maana, uhusiano na hali. Tatu mtafiti aliunganisha misimbo iliyolandana ili kuunda sura fulani ya kimaudhui.

## 3.0 MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa maktabani ili kukidhi lengo la makala haya. Lengo kuu lilikuwa ni kuchanganua mazingira yaliyoukilia ujitokeza wa matendo uneni katika tamthiliya teule.

**Jedwali Na.1: Mazingira ya Ujitokezaji wa Matendo Uneni katika teule**

| **Tamthiliya ya *Kuvuli Kinaishi*** | **Ukurasa** | **Tamthili ya *Nguzo Mama*** | **Ukurasa** | **Aiana ya Mgizingira** |
|---|---|---|---|---|
| **Mfano wa Mazingira** | | **Mfano wa Mazingira** | | |
| **a) BAWABU II: (***Anapowaona wanaginingi anasimama kwa hasira na kuwakabili huku rungu lake analizungushazungusha mkononi*).<br><br>Sheria ni sharia…nyote nyinyi mnaijua. Kila mmoja wenu akifika hapa natakiwa aeleze alichofanya mchana kutwa: kibaya au kizuri. Hamna kuficha……... Uk, 17 | 17 | **BI MOJA:** Huyo Bi Tano mwacheni. Kichwa chake kibovu. Jamani saa imekwisha. Hebu tugawane hivi ***vitambaa*** kila mtu akauze katika eneo Lake.<br><br>(***Wote wanagawiwa vitamba***). uk 17 | 17 | Mazingira ya Kuwepo kwa Vifaa Maalumu**.** |
| **b) BI. KIREMBWE:** Fungua tena kinywa. (*Mtolewa anafungua tena kinywa*) Nakuongezea tena unga wa ndere nikuweze. (*Anamshindilia nao kwa nguvu zaidi mara hii*) Huo…umeze…huo ugugubie… (***Kisha anamwonyesha rangi rangi nyeupe***) Sema hii nyeupe au nyeusi? Uk 53<br><br>**BI. KIZEE:** Mkimzungumzia mtu mkisema lolote kuhusu Giningi, (***Ananong'ona***) litakalokufikeni Mimi simo! (*Sasa anawawekea mkono wa kuume machoni watoto kwa zamu. Kila mtoto akishawekewe mkono na kuondolewa arudi nyuma kimbelembele bila ya kugeuka nyuma na kuketi pembeni.*) uk, 9 | 53<br><br>9 | **BI TANO:** Wee Bi Sita mshenzi. Unanichukulia mume wangu wangu hivi hivi kimachomacho. **[*MAGANGA anaondoka upesi upesi*] uk 35**<br><br>**BI SITA** [***Anamshika vizuri zaidi***]: Sikiliza nikwambie maana yake wewe ni mdogo wangu. Lile dume lako sina haja nalo. Hata ukinipa bure silitaki. Lile si demu. Katulize akili. [***Anamwachia. Anaondoka.***] Dume Malaya si dume roho yako kasumbua. Uk 36 | 35<br><br>36 | Mazingira ya Kuwepo kwa Lengo |
| **c) BI. KIREMBWE:** (Kwa Mtolewa) Inama…piga goti tukurambishe unga wa ndere ili tukugeuze…tukurambishe pepo wako kichwani alingane na pepo wa Giningi…52<br><br>**MTOLEWA:** Sawa baba…sawa mama…nimekuja maskusud munigeuze, nje ya Giningi kumoto hakukaliki hakuna vinono, hakuna marupurupu, hakuna vitanda vya maua… Niko tayari kufanya mtakavyonambia…uk 52 | 52 | **BI TANO:** Wee Bi Sita mshenzi. Unanichukulia mume wangu wangu hivi hivi kimachomacho.<br><br>**[*MAGANGA anaondoka upesi upesi*] uk 35** | 35 | Mazingira ya kuwepo kwa Hadhi na Mamlaka ya Msemaji |
| **d) KIREMBWE:** Fungua tena kinywa. (*Mtolewa anafungua tena kinywa*) Nakuongeza tena unga wa ndere nikuweze. uk 53 | 53 | **SUDI** (Kwa BI PILI): Haya nipe pesa ulizokwishapata.<br>**BI PILI:** Hee! Kwa nini nikupe?<br>**SUDI:** Wacha mdomo, nitakupiga mbele ya hawara zako (***anamshika***) uk 13-14 | 13-14 | Mazingira ya kitendo kutokea katika Wakati Muafaka wa Tamko |

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Nguzo Mama* (2007)

### 3.1.1 Mazingira ya Vifaa Maalumu vya Utendekaji

Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* data za utafiti zilionesha kwamba vifaa ni kitu muhimu katika kuwezesha ukamilifu wa kitendo uneni. Kwa mfano, uchoraji wa taswira za wahusika na mandhari. Vifaa hivi viliwezesha kufunua tabia za wahusika, hadhi zao kijamii na hata kusisitiza muktadha husika. Katika makala hii data ifuatayo inathibitisha jambo hili. Mwandishi anasema;

**BAWABU II:**

(*Anapowaona wanaginingi anasimama kwa hasira na kuwakabili huku rungu lake analizungushazungusha mkononi*).

Sheria ni sharia…nyote nyinyi mnaijua. Kila mmoja wenu akifika hapa anatakiwa aeleze alichofanya mchana kutwa: kibaya au kizuri. Hamna kuficha…... Uk, 17

Katika nukuu hii, data inaonesha kwamba kuna kitendo uneni cha amri kinachojitokeza katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* kwa kuwepo na kifaa maalum ambacho ni "**rungu**" analolitumia BAWABU II kuwa amrisha na kuwatishia Wanaginingi waliokuwa wanaingia Giningi. Ambapo baada ya kuzungushazungusha "**rungu"** lake ananena na kutenda tendo ambalo ni kuzungusha "rungu" ambapo usemi huu umefanikiwa pale ambapo wanaginingi wanasema ukweli wa yale waliyoyafanya na wanayotarajia kufanya. Aidha, kama ilivyo katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* lakini pia hata katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* data za utafiti zinathibitisha jambo hili kwa kuhusisha vazi la vitambaa ambavyo vimehusishwa katika uibuaji wa kitendo uneni cha maelekezo kama ifuatavyo;

**BI MOJA:**

Huyo Bi Tano mwacheni. Kichwa chake kibovu. Jamani saa imekwisha. Hebu tugawane hivi ***vitambaa*** kila mtu akauze katika eneo Lake.

(***Wote wanagawiwa vitamba***). uk 17

Nukuu hii data inaonesha kuwepo kwa kitendo uneni cha maagano ambacho ujitokezaji wake unazingatia kuwepo kwa vazi maalumu ambalo ni vitambaa vilivyokuwa vikiuzwa na akina mama waliokuwa wanapambana dhidi ya kujitegemea na kujipatia kipato. Ambapo kitendo uneni cha maagano huthibitishwa na data inayoonesha kwamba BI MOJA alitoa maelekezo mara baada ya kuzungumza walitenda kitendo ambacho ni kugawiwa vitambaa.

### 3.1.2 Mazingira ya Wakati Muafaka wa Mpokeaji usemi

Muafaka ni kipindi kinachofaa au cha haki kufanya jambo fulani. Katika uchunguzi huu, data za utafiti zilionesha kuwa kitendo uneni hutokea pale ambapo msikilizaji au mpokeaji wa tamko hilo anaweza kulitenda kulingana na wakati muafaka. Kwa mfano dondoo lifuatalo linadhihirisha hali hiyo:

**Mfano Na.1**

BI. KIREMBWE: Wakati umefika…. (***Anakwenda huku akirud huku***) Saa imefika… dakika imefika…nukta imefika…Mzimu unadai kulishwa…mabweha wanata ka mafungu yao… waganga na wachawi wanauliza mafigu yao…wachawi wanaitiliza kisasi chao….mwenye makosa afanywe nini?

WARI WOTE: Ahukumiwe… **(*Kwa sauti ya juu*).** uk 65

**Mfano Na. 2 BAWABU I:**

Jibu lako linanionyesha ulijitayarisha vyema. Sasa naanza kuona kwamba kadi hii uliipata kihalali… sasa piga hodi. Piga hodi mara tatu tu usizidi. Sema…

MTOLEWA: Hodi…hodi…hodi mara tatu… uk 15

**MTOLEWA:**

Wacha nijifundue. (*Anajifundua fedha kibindoni; yapata shilingi elfu tano hivi*) Maslahi kwa maslahi, shilingi elfu tano…"uk 28.

Katika nukuu hii **mfano Na.1** data zinaonesha kuwa mpokea usemi sharti awe na muafaka ambao ni kipindi kinachofaa/haki kufanya jambo. Kupitia nukuu hii data inaonesha kuwa BI. KIREMBWE ni mtoa usemi ambapo mpokea usemi ni WARI WOTE ambao ni sharti wawe na muafaka kuhusu usemi na muafaka huo ni kuitikia usemi wa BI. KIREMBWE kulingana na matakwa yake kwani ilikuwa ni lazima wapokea usemi kufanya hivo kwani ndo walikuwa wanapaswa kufanya hivo bila kupinga.

Pia, katika hoja hii **mfano Na.2** kulingana na uchanganuzi huu MTOLEWA ndiye mwenye muafaka kutokana na usemi ambao ulitolewa na BAWABU I na data ya utafiti ilionesha kuwa MTOLEWA ni mwenye muafaka kwa sababu ndie aliyekuwa anauhitaji wa kuingia Giningi. Hivyo, pamoja na kwamba kuna usemi ambao ulimfanya yeye afikie muafaka ambao ni kupiga hodi kwa kadri alivyoelekezwa lakini pia ilikuwa ni nafasi nzuri kwake kufanya hivyo kwasababu ya matamanio ya kuingia Giningi. Aidha, hata alipoombwa pesa, aliweza kutoa shilling elfu tano kama rushwa ili kuingia Giningi. Mwandishi anaeleza kuwa:

**BI MOJA:**

Huyo Bi Tano mwacheni. Kichwa chake kibovu. Jamani saa imekwisha. Hebu tugawane hivi ***vitambaa*** kila mtu akauze katika eneo Lake.

(***Wote wanagawiwa vitamba***). uk 17

Suala la kuwa na muafaka kwa mpokea usemi linaonekana katika data ambayo imepelekea kutokea kwa kitendo uneni cha maelekezo. Kwa kuonesha jinsi ambavyo BI MOJA alivyotoa usemi ambao ulipelekea wote kufikia muafaka ambao ni kugawiwa vitambaa kisha kwenda kuuza. Aidha, kitendo cha BI. MOJA kunena vile na kutekeleza jambo lile kutokana na kwamba muda ulikuwa umeenda kugawiwa vitambaa ilikuwa ndo muafaka wa usemi husika.

### 3.1.3 Mazingira ya Lengo Maalumu

Kitendo uneni hukubalika iwapo lengo la tamko linadhihirika wazi kwa wasikilizaji na utekelezaji wake na kusiwe na ugumu ikiwa na maana kwamba tamko linapaswa kuwa na manufaa kwa wasikilizaji au liwe linaweza kuibua athari fulani kwa wasikilizaji. Katika tamthiliya *Kivuli Kinaishi* mwandishi anasema;

**Mfano Na.1 BI. KIREMBWE:**

Fungua tena kinywa. (*Mtolewa anafungua tena kinywa*) Nakuongezea tena unga wa ndere nikuweze. (*Anamshindilia nao kwa nguvu zaidi mara hii*) Huo…umeze…huo uggubie…..uk, 53

**Mfano Na.2 BI. KIZEE:**

Mkimzungumzia mtu mkisema lolote kuhusu Giningi, (***Ananong'ona***) litakalokufikeni Mimi simo! (*Sasa anawawekea mkono wa kuume machoni watoto kwa zamu. Kila mtoto akishawekewe mkono na kuondolewa arudi nyuma kimbelembele bila ya kugeuka nyuma na kuketi pembeni*.) uk, 9

Katika **mfano Na.1** unaonesha kwamba kuna mazingira ya kuwapo kwa lengo la mtoa tamko katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi.* BI. KIREMBWE ambaye unenaji wake na utendaji uliofanywa kutokana na usemi/tamko lake ilikuwa na lengo la kumdumaza akili za MTOLEWA. Alilenga kufanya akili ya MTOLEWA isiweze kufukilia kuhusu kufanya mapinduzi wala kuhoji kuhusu uongozi mbaya katika nchi ya Giningi. Pia, **mfano Na.2** katika nukuu hapo juu, data inaonesha jinsi nambavyo kitendo uneni hujitokeza katika mazingira msemaji huwa na lengo fulani. Ambapo, data huthitisha hilo kwa kuonesha namna ambavyo mwandishi alivyomtumia muhusika BI KIZEE ambayo maneno na matendo yake yaliibua kitendo uneni cha maelekezo ambacho lengo lake ni kuwafumbua macho na akili watoto kwa kuwambia ukweli kuhusu maovu ya viongozi wanaotawala Giningi. Kwa upande wa tamthilia ya *Nguzo Mama*, mwandishi anadokeza,

**Mfano Na.1** BI TANO:

Wee Bi Sita mshenzi. Unanichukulia mume wangu wangu hivi hivi kimachomacho. [*MAGANGA **anaondoka upesi upesi***] uk 35

**Mfano Na.2** BI SITA [***Anamshika vizuri zaidi***]:

Sikiliza nikwambie maana yake wewe ni mdogo wangu. Lile dume lako sina haja nalo……. [***Anamwachia. Anaondoka.***] uk 36

**Mfano Na.1** data inaonesha kwamba usemi na tendo lililofuata ni dhahiri kwamba katika mazingira yale BI SITA alikuwa na lengo la kutamka usemi ule ambapo BI PILI alikuwa na lengo la kumfanya BI SITA na Mume wake BI TANO wabaini kwamba ameshagundua kuwa MAGANGA anamsaliti kwa kumtaka BI SITA. Katika data hii MAGANGA alitenda kitendo cha kuamua kuondoka kutokana na kwamba mke wake alikuwa tayari ashamgundua. Vilevile, katika **mfano Na.2** data inaonesha kwamba kuna mazingira maalumu ambayo yalipelekea BI SITA kutoa usemi kwa lengo la kumfanya BI TANO asiendelee kufikiria kwamba anaweza kuwa na mume wake kimapenzi. Hasa pale BI SITA alipoamua kumzungumzia vibaya MAGANGA ambaye ni mume wa BI TANO.

### 3.1.4 Mazingira ya kihadhi na Mamlaka ya Msemaji

Katika sharti hili, data zinaonesha kwamba hadhi na mamlaka ya mseamji ni uwezo na nguvu ya kisheria, kiutendaji au kijamii alizopewa mtu kumwezesha kuzungumza au kutenda jambo kwa niaba ya kundi fulani au taasisi. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* data zinaonesha kuwapo kwa hali hiyo kama mwandishi anavyosema katika dondoo lifuatalo:

**Mfano Na.1** BAWABU II:

(*Anapowaona wanaginingi anasimama kwa hasira na kuwakabili huku rungu lake analizungushazungusha mkononi*).

Sheria ni sharia…nyote nyinyi mnaijua. Kila mmoja wenu akifika hapa natakiwa aeleze alichofanya mchana kutwa: kibaya au kizuri….uk, 17

**Mfano Na.2** BI. KIREMBWE:

(Kwa Mtolewa) Inama…piga goti tukurambishe unga wa ndere ili tukugeuze…tukurambishe pepo wako kichwani alingane na pepo wa Giningi…

**MTOLEWA:**

Sawa baba…sawa mama…nimekuja makusudi munigeuze, nje ya Giningi kumoto hakukaliki hakuna vinono, hakuna marupurupu, hakuna vitanda vya maua…. Niko tayari kufanya mtakavyonambia…uk52

Katika **mfano Na.1** hapo suala la hadhi na mamlaka limethibitishwa na BAWABU II mlinzi. BAWABU aliwaruhusu watu wanaotaka kuingia Giningi na ndio maana data inaonesha kwamba alipowaona wanaginingi alianza kuzungushazungusha rungu lake kisha kufuatisha maneno ambayo ni kuwafanya waogope na waweze kutoa chochote kitu. Pia, jambo hili lilithibitika katika **mfano Na.2** hasa pale data zilipoonesha kwamba katika mazungumzo au majibizano lazima kuna mazingira ambayo yatadhihirisha kuwepo kwa mtu ambaye ni mwenye hadhi na mamlaka fulani kutokana na mazungumzo yanayotawala katika mazingira hayo. Aidha, katika nukuu hapo juu uchanganuzi unaonesha kwamba BI. KIREMBWE hutoa maelekezo kwa MTOLEWA katika tamthiliya ya *Nguzo Mama*.

**BI TANO:**

Wee Bi Sita mshenzi. Unanichukulia mume wangu hivi hivi kimachomacho. [***MAGANGA anaondoka upesi upesi***] **uk 35**

Kama data zinavyoonesha ni kweli kwamba katika nukuu hii, BI TANO ni mwenye hadhi na mamlaka ya kukaripia au kumgombeza BI SITA kwa sababu ilikuwa sio jambo la busara BI SITA kuingia kwenye mahusiano na MAGANGA kwani tayari ni mme wake BI TANO. Kwahiyo, kunena kwa BI TANO kisha MAGANGA afanya mwitiko kwa kuondoka upesi mahali pale ni uthibitisho wa kuwepo kwa kitendo uneni kilichodhihirisha au ibua mazingira ya kuwepo kwa hadhi na mamlaka ya mtoa usemi husika.

## 4.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti unaohusu ujitokezaji wa matendo uneni katika

tamthiliya teule. Mjadala huu umeongozwa na mapitio ya wataalam mbalimbali pamoja na nadharia ya Kitendo uneni iliyoasisiwa (1962) na Austin.

**4.1 Mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya teule.**

Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa kuna mazingira mbalimbali ambayo yamepelekea matendo uneni kutokea katika tamthiliya teule. Matokeo hayo yaliongozwa na nadharia ya kitendo uneni kwa kuzingatia muhimili wa pili ambao unasisitiza kuhusiana na jinsi muktadha wa tamko hudokeza msingi wa maana ya tamko lenyewe. Hata hivyo, waandishi huyafanya mambo ya kawaida kuonekana mapya kwa kuhusisha matendo uneni katika kazi zao. Kwa kumnukuu Mukarovisky (1990) anasisitiza kuwa kila siku lugha malengo yake nikuibua mawasiliano ya kila siku kwa kufanya kilichozoeleka kwa kukitumia kama mtindo ambao haujazoeleka ili kuonesha upya wa jambo linalozungumziwa katika miktadha tofauti.

Kwa kuzingatia matokeo hayo ni wazi kwamba mazingira ni msingi katika kazi za fasihi na uteuzi wa matumizi wa matendo uneni hutegemeana na mwaandishi anakusudia kuwasilisha jambo gani kwa jamii inayomzunguka. Ambapo, matendo uneni hutumika kama njia moja wapo ya kuonesha ubunifu wa mtumizi wa kazi husika kwa kutumia matendo uneni yanayotokana na mazingira tofauti kama njia ya kuibua dhamira kwa msomaji. Kwa kuzingatia hayo, ni dhahiri kwamba matokeo yameonesha matendo uneni yalibainika katika mazingira mbalimbali katika tamthiliya teule kama ifuatavyo;

*Mosi,* matokeo yamebaini kuwa mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni husababishwa na kuwepo kwa vifaa maalumu ambavyo hupelekea utamkwaji wa usemi fulani. Data hizi zimeakisi kuwa mazingira hayo yamepelekea kutokea kwa kitendo uneni cha amri ambacho huhusisha vifaa ambavyo vinatumika katika kutekeleza tendo husika. Matumizi ya tendo uneni yanayoibua mazingira ya utamkaji wenye amri kama yalivyodhihirihswa na Mohammed (1990). Amri hizo ni kama kuogofya, kutisha, kukemea, kulazimisha vilizokuwa zikitumiwa na Bawabu.

Utokeaji wa mazingira haya huibua hofu inayotokana na amri zinazotumiwa na wahusika katika *Kivuli Kinaishi*. Nadharia ya kitendo uneni inaelekeza kuwa kitendo uneni huweza kutokea pale ambapo kuna usemi/tamko ambalo hupelekea tendo fulani kutendeka kwa kuhusisha kuwa muktadha wa tamko hudokeza msingi wa maana ya tamko lenyewe. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa vifaa maalumu huweza kupelekea kutokea kwa kitendo uneni cha amri hasa pale ambapo vifaa hivyo vinapotumika kutoa amri kwa kuonesha vitisho kwa mpokea usemi husika.

*Pili*, mazingira ya kuwepo kwa lengo maalum, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna mazingira maalumu ambayo hupelekea kutokea kwa kitendo uneni cha amri. Ambapo amri hudhihirika pale ambapo mtu anamlazimisha mtu mwingine kufanya kile kinachoendana na kusudio lake. Matokeo haya yanathibitishwa na mawazo ya Brown na Yule (1993) ambao wanaeleza kwamba utambuzi wa msikilizaji wa nia/lengo la mzungumzaji ndio unaoonyesha ni aina gani ya kitendo uneni inayokusudiwa katika usemi. Wanaendelea kusema kwamba tamko linaweza kukaa kimaumbo kama swali ilihali kinachokusudiwa ni ombi. Pia, nadharia ya kitendo uneni inaweka wazi kuwa kitendo uneni hutokea pale ambapo mzungumzaji hukusudia kuibua athari fulani kwa kumfanya msikilizaji atambue nia yake ya kuibua athari hiyo. Kutokana matokeo ya utafiti ni wazi kwamba lengo ni msingi wa kutokea kwa kitendo uneni kwani usemi/tamko hutolewa na mtu akiwa analengo maalumu ambapo usemi unaotolewa ndio unaoonesha ni lengo gani mtao usemi amekusudia litendeke.

*Tatu,* mazingira ya wakati muafaka. Katika makala haya matokeo yanaonesha kuwa mazingira ya kuwapo kwa wakati muafaka hupelekea kutokea kwa kitendo uneni cha amari. Ambapo, Fromkin na Rodman (1988) wanaeleza kuwa wakati muafaka ni muda ambao ni sahihi au unaofaa kufanya jambo fulani. Wanaendelea kwa kusema kuwa wakati ni muda unaotambulika kuwa ni bora zaidi au unafaa katika kiutenda jambo au kufanya maamuzi fulani. Pamoja na hayo mazingira haya hutumiwa na waandishi katika kazi zao katika kuwasilisha kile ambacho wamekusudia kukifikisha kwa jamii lengwa. Aidha, katika mazingira ya kuwapo kwa wakati muafaka dhamira mbalimbali kama vile; *kudumaza, unyanyasaji, mapinduzi* na *uzalendo* hudhihilishwa na waandishi katika zao.

*Nne,* mazingira ya kihadhi na mamlaka ya msemaji, katika makala haya matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba mazingira ya hadhi na mamlaka ya msemaji hupelekea kutokea kwa kitendo uneni cha amri, hisia na maelekezo. Pia, nadharia ya kitendo uneni inaweka wazi kwamba nguvu za tamko huonyesha kuwa mzungumzaji na msikilizaji ni washiriki kwa kumuonesha mtoa usemi kuwa ndiye mwenye mamlaka ya kutekeleza suala fulani. Aidha, Mohamed (1990) na Penina (1982) katika kazi zao wanaonesha kuwa hadhi na mamlaka ni mazingira maalumu ambayo mtoa tamko huwa ndie mwenye nguvu na uwezo wa kufanya maamuzi au kuthibiti watu au jambo fulani. Hii inamanisha kwamba kitendo uneni cha amri, hisia na maelekezo hutokea pale ambapo kuna mazingira maalumu ambayo huomesha kuwepo kwa hadhi na mamlaka ya mtoa usemi/tamko. Kwa maana hiyo, waandishi wa kazi za kifasihi hujikuta wakitumia matendo uneni katika mazingira tofauti tofauti kwa lengo la kufanya kazi zao kufikia katika kilele cha ukubalifu hasa kwa kuwasilisha vema ujumbe kwa jamii lengwa/iliyokusudiwa.

## 5.0 HITIMISHO

Makala hii imechanganua mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya teule. Lengo mahususi ikiwa ni kuchanganua mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya teule. Matokeo yemedhihirisha mazingira manne ya ujitokezaji wa mtendo uneni. Pamoja na kuwepo kwa mazingira hayo ya ujitokezaji wa matendo uneni kama yalivyobainishwa katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti na mjadala wa matokeo ya utafiti ni wazi kwamba matokeo ambayo yameonesha kuwapo kwa mazingira tofauti tofauti, mazingira hayo yamepelekea kuibuka kwa kitendo uneni cha amri kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na jinsi ambavyo mazingira hayo yalivyoibua matendo uneni mengine kama vile; matendo uneni ya maelekezo, hisia, maagano na majigambo. Kwa upande mwingine, inaonekana kuwa mazingira huweza kuchipua matendo uneni ya aina mbalimbali kutokana na namna mwandishi alivyoamua kuwasilisha kazi yake kwa jamii lengwa. Hivyo, kupelekea jamii kupata ujumbe/dhamira tofauti tofauti na kwa weledi zaidi. Pamoja na hayo yote ni vema tafiti mbalimbali zifanyike zinazohusisha matendo uneni/mazingira ya ujitokezaji wa matendo uneni katika tamthiliya za waandishi wengine ili kuweka bayana athari na dhima mbalimbali ambazo huweza kuibuliwa na mtendo uneni yanayojitokeza kutokana na mazingira maalumu.

## MAREJELEO


- Austin, J. L. (1962). *How to do Things with Words*. London: Oxford University Press.
- Brown, G., & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Fromkin, V., & Rodman, R. (1988). *An Introduction to Language*, 4th Edition, New York: Holt, Rinehart and Winston Inc.
- Grice, H. P. (1990). *Logic and Conversation*. In: The Philosophy of Language, edited by A.P. Martinich. Oxford: OUP.
- Matasi, B. (2014). Uchanganuzi wa Vitendoneni katika Khutuba za Ijumaa na Athari zake Kwa Waumini wa Bagisu, Mashariki mwa Uganda. *Chuo kikuu Cha Egerton. Haijachapishwa*.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa sekondari, Vyuo vya kati na Vyuo vikuu*. Mwanza: Serengeti Education Publishers Ltd.
- Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mukarovisky, J. (1990). Standard Language and Poetry Language. Washton DC: Georgetown University press.
- Ogolla, A. R. (2007). Uchanganuzi wa Jinsi Lugha Inavyotumika Kuhamasisha Wanawake kuhusu Haki Zao: Mfano kutoka Wilayani Kisumu. *Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton*.
- Panneerselvam, R. (2007). *Research Methodology*: New Delhi. Prentice Hall.
- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi:* Dar es salaam. Karjaner Print Techinology.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Resani, M. (2014). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Saalam: Karjamer Publisher.
- Searle, J. R. (1975). *Speech Acts: An Essay in Philosophy of Language*. New York: Cambridge University Press.
- Walya, E. (1995). *Discourse Strategies in Banking Discourse*. M.A. Thesis, Kenyatta University.


**Cite This Article:** Edson Limbuko Andrea & Dkt Neema George Mturo (2024). Mazingira ya Ujitokezaji wa Matendo uneni katika Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Nguzo Mama*. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 7*(12), 429-435.